**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI TANZANIA

**April , 2024.**
**Dodoma**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS – TAMISEMI**

**Shule ya Sekondari Nasuli**
**S.L.P 21.**
**NAMTUMBO-RUVUMA**
**Tarehe 12/04/2024**

**Mkuu wa Shule 0765978421**
**Makamu 0752331702**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ………….**
**……………………………………………..**
**S.L.P ……………………………………..**
**…………………………………………….**

YAH**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI NASULI HALMASHAURI YA NAMTUMBO MKOA RUVUMA MWAKA 2024/2025**

**i.** Ninafurahi kukutaarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha Tano katika shule hii kwa mwaka 2024/2025. Shule hii ipo kilometa 68 mashariki mwa mji mkuu wa mkoa wa Ruvuma (Songea) na Kilometa 185 magharibi mwa wilaya ya Tunduru mkoani Ruvuma. Usafiri wa Basi toka Songea mjini unapatikana kituo cha Mabasi Songea, nauli ni Tshs 4000/=. Ukifika Namtumbo teremka katika kituo kikuu cha mabasi cha Namtumbo na shule yetu ipo upande wa pili wa barabara. **UNATAKIWA KURIPOTI SHULENI KUANZIA TAREHE …………….. MPAKA ………………** Mwanafunzi atakae chelewa kuripoti kwa tarehe hiyo, nafasi yake atapewa mwanafunzi mwingine

**ii.**

**iii. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA :-**

**3.1 SARE ZA SHULE**

i. Shati nyeupe mbili mikono mifupi (Mashati mawili au zaidi)
ii. Sketi ya rangi ya Kijani iliyoiva (dark green) yenye rinda box mbele na nyuma yenye urefu Sentimita 15 toka unyayoni (Sketi fupi HAZIKUBALIKI). (ZINAPATIKANA SHULENI KWA ANAEHITAJI)
iii. Viatu vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi.
iv. Soksi nyeupe (jozi mbili).(zinapatikana shuleni(kwa anaehitaji)
v. Sweta la shule rangi ya kijani iliyoiva (dark green). (YANAPATIKANA SHULENI KWA ANAEHITAJI)Tsh 12000/=

vi. Nguo za kushindia, (Shamba dress) ni Gauni rangi ya damu ya mzee, mshono ni solo.Gauni ni Tsh 36000/=
vii. Sketi ya shule yenye urefu wa sintimeta 15 kutoka unyayoni.(ZINAPATIKANA SHULENI KWA ANAYEHITAJI Kwa Tsh27000/=
viii. Hijabu ifanane na sare za shule (Nyeupe na Damu ya mzee sio mtandio isiwe na urembo wala lessi).
ix. Kwa waislamu nguo ya msikitini ni -suruali dark blue ya heshima na isibane -nusu kanzu ndefu ipite magoti na yenye mikono mirefu
x. Sare ya michezo, traksuit nyeusi zenye michirizi nyeupe pembeni na raba nyeupe. Trak suit zinapatikana shuleni kwa Tsh 25000/= kwa Anayehitaji
xi. Tshirt za DAMU YA MZEE (zinapatikana shuleni kwa Tshs 15,000/= kwa atakae hitaji)
xii. Tshirt ya michezo moja(TAIFA STERS YA BLUE) INAPATIKANA SHULENI KWA ANAYEHITAJI

**3.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-**

i. Madaftari yasiyopungua 10 quire three kwaajili ya kutunzia notes nadaftari aina yoyote kwaajili ya mazoezi kwa kila somo. DAFTARI ZINAPATIKANA SHULENI.
ii. Mkebe wenye vifaa vya mahesabu. UNAPATIKANA SHULENI kwa Tsh 2000

iii. Kalamu za wino bluu/nyeusi, yaani 01 kila mhula, faili 01 kwa ajili ya kutunzia nyaraka zake, scientific calculator kwa wanaosoma masomo ya sayansi, dissecting kiti (kwa wanaosoma Biology) **na koti la maabara jeupe** ( kwa wanaosoma CBG na PCB)
iv. Aje na sanduku (sanduku la bati ) linalofunga vizuri kwa ajili ya kuhifadhia nguo zake na vitu vyake.
v. Aje na godoro la futi 21 / 2 kwa futi 6 pamoja na mto na foronya yake
vi. Aje na blanketi 01, shuka rangi ya bluu bahari 02, pinki 01, chandarua rangi nyeupe/bluu 01 na taulo 01.
vii. Kila mwanafunzi aje na **JEMBE MOJA (1)** pamoja na kifaa kimojawapo (01) kulingana na mkondo wake kama ifuatavyo:
- HGL-Kwanja 01
- HGE-kwanja 01
- PCB-Panga 01
- CBG-Panga 01

Fagio (chelewa) 02 na soft bloom 01, hard bloom 01na brashi ngumu 01yenye mpini mfupi kwaajili ya kusafishia sinki la choo

viii. Ndoo za lita kumi mbili (02) na Squeezer 01 kwa ajili ya kukaushia maji sakafuni
ix. Aje na matokeo ya kidato cha nne (result slip) na cheti cha kuzaliwa.

### 3.3 Michango mbalimbali Shule za Bweni

| Na | AinayaMchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

Fedha za michango zilipwe kwenye akaunti ya shule namba **62401100009** Jina la akaunti (NASULI SECONDARY SCHOOL) benki ya NMB (Tafadhali andika jina la mwanafunzi kwenye karatasi ya kuwekea hela (paying slip) na iletwe shuleni siku atakayoripoti mwanafunzi.

Aje na Tsh **50,400**/= kwa ajili ya bima ya afya kwa mwaka mzima (kwa wale ambao hawana bima ya afya). **BIMA YA AFYA NI LAZIMA** kwani itamsaidia kutibiwa kwa mwaka mzima sehemu yoyote nchini. (fedha hizo siyo sehemu ya michango ya shule, hivyo alete fedha taslimu. Asiingize kwenye akaunti ya shule)

### iv. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku(Night Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- ❖ **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shule ni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtu mishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**
- ❖ **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa.**
- ❖ **Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**
- ❖ **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).
- ❖ **KILA MWANAFUNZI LAZIMA AWE NA BIMA YA AFYA**

**3.2 Makosa yatakayo sababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupiga na mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababishamimba;
xiii. Kushiriki matendo yauhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayo vunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera yaTaifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**v. Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine ya na yotolewa na shule; na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

**vi.** Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**Saini ya Mkuu wa Shule …………………**
**Jina la Mkuu wa Shule**

**BULE ELIAH MWAIKENDA**

**Mhuri wa Mkuu wa Shule ………………………………..**

**NB:** **Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule 0765978421**
- **Makamu Mkuu wa Shule 0752331702**
- **Matroni 0711506053**
- **Mwandamizi Malezi 0713452298**